**Hotuba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza Katika Ufunguzi wa Mafunzo ya Mfumo mpya wa kuandaa Mipango na Bajeti za Mamlaka ya Serikali za Mitaa**

**Julai 24, 2017, Katika Ukumbi wa Victoria Palace Jiji Mwanza.**

**Mwakilishi kutoka OR-TAMISEMI,**

**Mwakilishi kutoka OR-Utumishi,**

**Mwakilishi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango,**

**Mwakilishi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto,**

**Wawakilishi kutoka PS3,**

**Wakufunzi wetu,**

**Waandishi wa Habari,**

**Ndugu washiriki, Mabibi na Mabwana.**

**Habarini za muda huu**

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kukutana hapa siku ya leo. Hii imekuwa nafasi ya pekee ambapo tumeweza kukutana kwa ajili ya mafunzo kwa watumiaji wa Mfumo ulioboreshwa wa kuandaa Mipango na Bajeti za Mamlaka ya Serikali za Mitaa uitwao PlanRep. Uboreshaji wa Mfumo wa PlanRep na Mafunzo haya yamewezekana kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma ujulikanao kwa Kiingereza kama *Public Sector Systems Strengthening,* (PS3). Mradi huu unafadhiliwa na Watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), na tunawashukuru sana.

Pili, naomba niwashukuru waandaaji wa mafunzo kwa heshima mlionipa ya kuja kufungua mafunzo haya ambayo yanakwenda kuboresha zoezi la uandaji wa mipango na bajeti katika Halmashauri zetu. Mfumo wa PlanRep ulioboreshwa pia unaenda kutumika kuanzia ngazi ya msingi yaani vituo vyetu vya kutolea huduma ambapo utawezesha kuandaa mipango na bajeti kutokana na vipaumbele na mahitaji ya wananchi ambao ndio waathirika wakubwa iwapo mipango na bajeti hizi hazitazingatia mahitaji yao. Kupitia nafasi hii maalum, mimi pia nitajifunza na kuona namna mfumo wa PlanRep ulioboreshwa.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Nimefahamishwa kwamba mafunzo haya kwa awamu ya kwanza yanafanyika katika kanda mbili, ambazo ni Mwanza na Mtwara, na kwamba yanajumuisha watumiaji wa mfumo huu ambao ni Waganga Wakuu, Makatibu wa Afya, Maafisa TEHAMA na Wachumi kutoka ngazi ya Mkoa kwa upande mmoja, pamoja na

Waganga Wakuu, Maafisa Mipango, Wahasibu, Wachumi, na Maafisa TEHAMA wa Halmashauri kwa upange mwingine. Watumiaji hawa ndio wahusika katika kuandaa mipango na bajeti za Halmashauri kutokana na taarifa zilizokusanywa kutoka vitengo mbalimbali ndani ya Halmashauri zao. Lengo la mafunzo haya ni kuwajengea uwezo wataalam wanaohusika katika mchakato mzima wa kuandaa mipango na bajeti za Halmashauri ili waweze kuutumia mfumo wa PlanRep kwa ufasaha na kuwajengea uwezo wataalam wengine ndani ya Mikoa na Halmashauri.

Ninafahamu kuwa, mafunzo haya yatakuwa ya siku nane, na yataendeshwa na timu ya wakufunzi iliyoundwa kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Fedha na Mipango, Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), Sekretarieti za Mikoa, PS3 pamoja na Wizara za Kisekta ikiwemo Wizara ya Afya.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Kupitia mfumo huu wa PlanRep ulioboreshwa unakwenda kuondoa na kutatua changamoto mbali mbali zilizokuwepo kwenye mfumo wa zamani. Mfano, kwa kutumia mfumo wa zamani wa PlanRep, huwezi kuainisha mipango na bajeti za kituo kimoja kimoja kwa kuwa mipango yote ilikua ikiishia kwenye ngazi ya Halmashauri. PlanRep hii iliyoboreshwa imefanyia kazi changamoto hii kwa kuhakikisha kwamba mpango na bajeti unaingizwa kwa kila mtoa huduma, na unaingiza namba za utambulisho kwa kila mtoa huduma mmoja mmoja kwa kila sekta. Vile vile, mfumo huu umeweka nafasi ya kila mtoa huduma

kuainisha matokeo yanayotegemewa (Service Outputs). Hii itasaidia watoa huduma kujipima kwa kuangalia matokeo katika utoaji wa huduma na hivyo kuweza kufanya tathmini ya thamani ya fedha (Value for money). Hivyo basi mfumo huu ulioboreshwa unakuja kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwenye sekta za umma.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Natambua kwamba kutokana na mabadiliko na kurahisishwa kwa teknolojia, mfumo huu mpya wa PlanRep nao umerahisishwa kwa kufanywa kuwa 'Web Based' hivyo utawezesha Halmashauri kuingiza taarifa za mipango na bajeti moja kwa moja kwa njia ya mtandao na kuweza kutumwa kwenye mfumo mmoja uliopo OR-TAMISEMI. Hili litawezesha kufanyiwa kazi ili kuingia kwenye bajeti kuu ya mwaka wa fedha husika, na itasaidia pia kutoa mrejesho wa mara kwa mara kwa ngazi zote za utawala kwa wakati.

Vilevile, uwezo wa mfumo huu kuingiza mipango na bajeti moja kwa moja, utapunguza gharama kubwa iliyokuwa ikitumika awali kwa kuhitaji wataalam kukusanyika eneo moja kwa ajili ya kuifanya kazi hiyo. Utaratibu wa awali ulitumia gharama kubwa, lakini pia ulisababisha wataalam hao kutokuwa katika vituo vyao vya kazi kwa muda mrefu, na hivyo kushindwa kuhudumia wananchi waliokuwa wakihitaji huduma kutoka kwao wakati huo wa uandaaji wa mipango na bajeti. Ni jambo la kujivunia sana kwamba kuanzia sasa, mipango na bajeti vitaendelea kufanyika katika vituo vya kazi, sanjari na kuendelea kumhudumia

mwananchi wa Tanzania kupata huduma anayostahili. Naomba tuwapongeze wataalam wote waliohusika katika kulifanikisha hili.

Katika hili pia, naomba tu nitoe angalizo kwamba hakutakuwa na kisingizio cha kutokuwepo kwa mtandao katika halmashauri zetu, kwani wenzetu wa PS3 hivi sasa wapo katika zoezi la kufunga mitambo ya intaneti (Local Area Network – LAN) katika Halmashauri 93 zilizo chini ya Mradi. Hivyo tunatarajia kwamba kasi na ari ya kazi itaongezeka zaidi, kutokana na maboresho haya ya teknolojia. Nitoe rai pia, pale ambapo mtandao kiambo (LAN) haupo, basi Halmashauri husika itumie vyanzo vyake vya ndani kupata fedha za kugharamia ukamilishaji wa LAN kwa Halmashauri nzima.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Nimejulishwa kuwa, mfumo huu mpya unakwenda kutatua changamoto zote zilizokuwepo kwenye mfumo wa zamani ikiwemo uwepo wa matoleo mengi yanayotumiwa kwa wakati mmoja (Planrep versions); uwepo wa bajeti tofauti kwenye kila ngazi ya utawala kuanzia ngazi ya Halmashauri, Mkoa, Wizara za Kisekta, OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha; kutumia muda mwingi wakati wa upembuzi wa bajeti (budget scrutinisation); kutokungea kwa mifumo ikiwemo mfumo wa PlanRep na Mfumo wa Matumizi ya Fedha (IFMIS Epicor); uwasilishaji wa bajeti nje ya muda; uingizaji wa bajeti katika mfumo wa Epicor; Upatikanaji wa taarifa za mapato, mipango, bajeti na matumizi; uhusianishwaji wa bajeti za sekta zote na nyingine nyingi. Kwa kuwa mfumo huu umeboreshwa, na kwa kuwa mfumo huu ni mmoja kwa sekta zote na kwa kuwa wataaalam wanne ngazi ya

Mkoa na sita ngazi ya Halmashauri wanafundishwa, tunategemea kuona maboresho na mageuzi makubwa katika eneo la upangaji wa mipango, uandaaji wa bajeti na utoaji wa taarifa kwa wadau wote na ngazi zote za Serikali.

Ninafahamu pia kwamba kutakuwa na mafunzo ya mfumo wa kielektroniki wa uhasibu na utoaji taarifa za fedha, ambao kwa Kiingereza unajulikana kama Facility Financial Accounting Reporting System (FFARS). Mafunzo ya awali ya mfumo huu wa FFARS yalifanyika mwezi Juni mwaka huu, na tayari wahusika wa kuandaa mahesabu na utoaji wa taarifa katika ngazi ya kituo wamekwishafundishwa. Naomba niwasisitizie nyie mtakaofundishwa mfumo huu wa FFARS, muende kuwafundisha wahusika watakaokuwa wakiutumia mfumo huu moja kwa moja kwenye ngazi ya msingi ya watoa huduma. Mafunzo ya mfumo wa FFARS yana umuhimu wa kipekee kutokana na mfumo huu kuwezesha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha katika ngazi ya kituo, na hivyo kusaidia kufikia malengo ya utoaji huduma, pamoja na kuhakikisha yanaendana na sheria na taratibu za manunuzi na utoaji taarifa. Taarifa hizi zitasaidia Serikali kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Umma na kuongeza uwazi, na hivyo watoa huduma kuwa na wajibu kwa jamii wanayoihudumia.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Naomba nimalizie kwa kuchukua fursa hii kuwashukuru sana PS3 kwa mafunzo haya, maana kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) ambao tayari wamekuwa wanafanya kazi kwa karibu sana na Serikali ya Tanzania. Tangu Mradi huu umeanza kutekelezwa, tumeshuhudia mafanikio kila siku, na utendaji kazi wetu katika Mikoa na Halmashauri

umeboreshwa kutokana na mifumo yetu kuendelea kuimarishwa. Ni jambo la kheri sana katika nchi yetu, na tunatarajia kwamba mpaka kufikia mwisho wa utekelezaji wa Mradi huu mifumo mingi itakuwa imeboreshwa, na hivyo kufanikisha kuwa na Tanzania yenye neema zaidi.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Baada ya kusema haya, naomba nitamke kwamba Mafunzo haya ya watumiaji wa **Mfumo mpya wa kuandaa Mipango na Bajeti za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, yamefunguliwa rasmi.**

Nawatakia mafunzo mema, na Asanteni kwa kunisikiliza.